**TANGAZO**

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania anapenda kuwatangazia wakulima wote wa zao la korosho kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, na Pwani kuwa zoezi la kuhuisha taarifa za mashamba ya korosho limeanza rasmi tarehe 17 Februari, 2025 na mwisho ni tarehe 31 Machi, 2025.

**MAHALI:** Ni Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji lilipo shamba la mkulima.

**SIKU NA MUDA WA KUHUISHA TAARIFA:**

Ni kila siku kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi; kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni.

**KILA MKULIMA ANATAKIWA KWENDA KUHUISHA TAARIFA ZAKE AKIWA NA:**

- Kitambulisho cha NIDA au cha Mpiga Kura
- Namba yake ya simu ya mkononi
- Namba ya Mkulima wa Korosho aliyoitumia msimu uliopita

⚠️ **ANGALIZO MUHIMU:** Mkulima yeyote atakayeshindwa kuhuisha taarifa zake ndani ya muda uliopangwa, hatopata pembejeo zinazotolewa bure na Serikali kwa msimu wa mwaka 2025/2026.

Kwa maelezo zaidi, fika katika Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji lilipo shamba lako, au tupigie simu kwa nambari ***0 8 0 0 1 1 2 1 5*** **9**.

***Usikiapo Tangazo hili mtaarifu na mwingine.***

**Tangazo hili limetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania**